

# HALMASHAURI YA MJI WA KONDOA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Halmashauri ya Mji wa Kondoa)

Simu: +255 712264912

Mkurugenzi wa Mji

Nukushi: +255 262360313

S.L.P 711,

Barua pepe: [td@kondoatc.go.tz](mailto:td@kondoatc.go.tz)

KONDOA.

Tovuti: [www.kondoatc.go.tz](http://www.kondoatc.go.tz)



## TAARIFA YA IDARA YA ELIMU MSINGI

### 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Mji Kondoa ina jumla ya shule za Msingi (29) ishirini na tisa, kati ya hizo (26) ishirini na sita ni za Serikali na (3) tatu ni za Binafsi.

Katika shule za Serikali kuna Jumla ya wanafunzi 14662, kwa darasa la kwanza hadi darasa la saba kati yao wavulana na 7276 na wasichana ni 7386, shule binafsi zina jumla ya wanafunzi 673, ambao wavulana ni 340 na Wasichana ni 333 kwa darasa la kwanza hadi darasa la saba.

Idara ya Elimu Msingi ina jumla ya walimu 107, kati yao wanawake ni 230 na wanaume ni 337, hata hivyo Idara ina upungufu wa walimu wa kufundisha madarasa ya awali.

### 2.0 MAWASILIANO YA WATUMISHI WA IDARA YA ELIMU MSINGI

Idara ya Elimu Msingi ina Jumla ya watumishi watano na mawasiliano yao ni kama inavyoonekana kwenye jedwali:-

SN	JINA LA AFISA	CHEO	NAMBA YA SIMU
1.	George J. Lukoa	Kaimu Afisa Elimu Msingi Mji (TPEO)	0712 - 580273 <a href="mailto:lukoag@gmail.com">lukoag@gmail.com</a>
2.	Onael Nyange	Afisa Elimu Vifaa na Takwimu (SLO)	0756 - 795426 <a href="mailto:onaelnyange@yahoo.com">onaelnyange@yahoo.com</a>

3.	Joyce Mwajombe	Afisa Elimu Taaluma (TSAO)	0718 - 010174 <a href="mailto:Mwajombe.joyce@yahoo.com">Mwajombe.joyce@yahoo.com</a>
4.	Kanasia Nyella	Afisa Elimu Kilimo	0756 – 300372 <a href="mailto:kananyella@gmail.com">kananyella@gmail.com</a>
5.	Adray Kikoti	Afisa Elimu Vielelezo	<a href="mailto:lazaroadray@gmail.com">lazaroadray@gmail.com</a> 0785 – 365527

## 2.0 KAZI ZA IDARA

Idara ya Elimu Msingi ndiyo yenyeye dhamana na kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu elimu Msingi katika Halmashauri ya Mji Kondoa. Shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuratibu shughuli zote zinazohusu taaluma katika Halmashauri
- ii. Kusimamia utendaji kazi wa walimu na watumishi wa idara ya Elimu na wasio kuwa walimu.
- iii. Kuratibu takwimu zote za Idara ya Elimu kama vile Miundombinu ie vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, n.k, idadi ya wanafunzi, walimu na nyinginezo.
- iv. Kuratibu Maslahi ya walimu kama likizo, madai mbalimbali kama vile uhamisho, mizigo na malimbikizo ya mishahara pamoja na kupanda madaraja.
- v. Ulinzi na usimamizi wa mali za Umma zitumikazo katika Uendeshaji wa Elimu msingi kama vile Samani za shule, maeneo ya shule na mali nyingine.
- vi. Kudhibiti utoro wa walimu na wanafunzi na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria, taratibu na Kanuni za Elimu na nchi kwa ujumla

## 4.0 HUDUMA ZINAZOTOLEWA KATIKA IDARA YA ELIMU MSINGI

Idara ya Elimu Msingi inatoa huduma mbalimbali zinazohusiana na mambo ya Elimu na Taaluma kwa wanafunzi, wananchi na Walimu kwa ujumla. Vilevile Idara hii hutoa huduma kama inavyoelekezwa na Mkurugenzi wa Halmashauri Katibu Tawala Mkoa na Viongozi

mbalimbali wananchi kwa kuzingatia miongozo, nyaraka na maelekezo mbalimbali. Baadhi ya Huduma zitolewazo ni kama ifuatavyo:

- i. Kushughulikia uhamisho wa wanafunzi na walimu
- ii. Kushughulikia likizo za walimu na watumishi na wasio walimu wanaohudumia katika Idara ya Elimu msingi
- iii. Kushughulikia masuala ya kinidhamu na utoro wa walimu na wanafunzi.
- iv. Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wazazi, wanafunzi na walimu kwa ujumla
- v. Maslahi ya walimu kama madaraja n.k
- vi. Huduma mbalimbali zinazohusiana na taaluma

## **5.0 MATARAJIO YA IDARA**

Idara inatarajiwa kufanya mambo yafuatayo:

- i. Kupandisha kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wanaofanya mitihani ya Taifa kama vile Mitihani ya Darasa la Nne na la Saba 80 – 95%.
- ii. Kuamsha ari ya utendaji kazi kwa walimu ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi.
- iii. Kujenga uhusiano mzuri baina ya walimu, wanafunzi na Jamii inayozunguka shule (wananchi)
- iv. Kuhakikisha maslahi ya walimu yanaboreshw na kupatikana kwa wakati kama vile fedha za likizo, uhamisho, kupanda madaraja kwa walimu, makazi bora ya walimu, upatikanaji wa vifaa vya kusomea na kufundisha kwa wakati.
- v. Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa Elimu na kuwapatia watoto elimu bora.

vi. Kuendesha vikao vya wadau wa Elimu katika Halmashauri ili kuleta tija katika elimu

## **HITIMISHO.**

Idara ya Elimu Msingi inatoa rai kwa walimu kufundisha, na kusimamia nidhamu za wanafunzi vilevile tunawaomba wazazi wawape ushirikiano walimu ili kuhakikisha watoto wanapata elimu bora.

- Wanafunzi wajitambue na kujua umuhimu wa Elimu kwao binafsi na kwa Taifa kwa Ujumla.
- Idara ya Elimu Msingi inatarajia kupitia elimu inayotolewa katika Halmashauri ya Mji Kondoa ili kupata Taifa bora na lenye kujitambua.

Nawasilisha

*George J. Lukoa*

**KAIMU. AFISA ELIMU MSINGI,**

**MJI KONDOA.**

**KARIBUNI WANANCHI KATIKA IDARA YA ELIMU MSINGI**

